

50

52



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA



DOKEZO SABILI

KWENDA KWA: MKURUGENZI MTENDAJI (W)

KUTOKA KWA: AFISA MALIASILI NA MAZINGIRA (W)

TAREHE: 26/10/2022

YAH: MRADI WA MIFUMO YA CHAKULA, MATUMIZI YA ARDHI NA UREJESHAJI
KATIKA MANDHARI YA MISITU YA TANZANIA

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

Mradi wa Mifumo ya Chakula, Matumizi ya Ardhi na Urejeshaji katika Mandhari ya Misitu ya Tanzania (FOLUR) ulioko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii utafanyika Wilaya ya Kilombero kwa Tanzania Bara na Wilaya ya Kaskazini A kwa upande wa Zanzibar. Mradi huu umepata ufadhili kutoka katika Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) chini ya Programu ya Mifumo ya Chakula, Matumizi Ardhi na Urejeshaji (FOLUR).

Kwa Mujibu wa Sera za Mfadhili (GEF), taarifa za Mpango wa Ushirikishaji wa Wadau na Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii & mfumo wa Mchakato wa mradi vinapaswa kuwekwa wazi kwa wadau. Kutokana na sababu hiyo tumepewa Nyaraka zinazoelezea Mpango wa Ushirikishaji wa Wadau na Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii & Mfumo wa Mchakato kwaajili ya mradi huu ili tuziweke kwenye Tovuti ya halmashauri kwaajili ya wadau kuzipitia na kupata uelewa kwa siku zisizo pungua 45.

Hivyo, ninawasilisha kwako nyaraka hizo ili uzipokee kama kumbukumbu ya halmashauri na kukuomba utoa maelekezo kwa wataalamu wa kitengo cha Tehama ili waziweke kwenye Tovuti ya Halmashauri.

Nawasilisha

Joseph E. Mgana
Afisa Maliasili na Mazingira (W),
MLIMBA.

